WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA
TAASISI YA ELIMU TANZANIA

MUHTASARI WA SOMO LA MAFUNZO KABILISHI NA MJONGEO KWA MWALIMU TARAJALI WA FANI YA ULEMAVU WA UONI

ASTASHAHADA YA UALIMU ELIMU MAALUMU

© Taasisi ya Elimu Tanzania, 2019

Toleo la Kwanza 2019

ISBN: 978-9976-61-840-2

Taasisi ya Elimu Tanzania
S.L.P. 35094
Dar es Salaam
Tanzania

Simu: +255 222 773 005
Faksi: +255 222 774 420
Baruapepe: director.general@tie.go.tz
Tovuti: www.tie.go.tz

Muhtasari huu urejelewe kama: Taasisi ya Elimu Tanzania. (2019). Muhtasari wa Somo la Mafunzo Kabilishi na Mjongeo kwa Mwalimu Tarajali Astashahada ya Ualimu Elimu Maalumu. Dar es Salaam: Taasisi ya Elimu Tanzania.

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kunakili, kurudufu, kuchapisha, kutafsiri wala kuutoa muhtasari huu kwa namna yoyote ile bila idhini ya maandishi kutoka Taasisi ya Elimu Tanzania.

Idhini

Mafunzo ya Astashahada ya Ualimu Elimu Maalumu ni ya miaka miwili na yamekusudiwa kumuandaa mwalimu tarajali kuwa mahiri na mwenye uwezo wa kufanya kazi kwa dhati na kwa weledi. Mwalimu huyo atafundisha katika shule za msingi zinazodahili wanafunzi wenye mahitaji maalumu. Mwalimu tarajali atatambuliwa kuwa ni mwalimu baada ya kuhitimu mafunzo ya Astashahada ya Ualimu Elimu Maalumu na kufaulu mafunzo ya nadharia na mafunzo ya ualimu kwa vitendo.

Muhtasari huu umeidhinishwa kuwa ni wa somo la Mafunzo Kabilishi na Mjongeo katika Mafunzo ya Astashahada ya Ualimu Elimu Maalumu.

Dkt. Lyabwene M. Mtahabwa
Kaimu Kamishna wa Elimu
Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia
S.L.P. 10
Dodoma

Simu: +255 262 963 533
Baruapepe: info@moe.go.tz
Tovuti: www.moe.go.tz

YALIYOMO

Idhini iii

1.0 Taarifa za Awali 1

1.1 Utangulizi 1

1.2 Muundo wa Muhtasari 1

1.3 Sababu za Kuandaa Muhtasari 2

1.4 Malengo ya Elimu Nchini Tanzania 2

1.5 Malengo ya Jumla ya Mafunzo ya Astashahada ya Ualimu Elimu Maalumu 3

1.6 Madhumuni ya Mafunzo ya Astashahada ya Ualimu Elimu Maalumu 4

1.7 Umahiri wa Jumla wa Mafunzo ya Astashahada ya Ualimu Elimu Maalumu 4

1.8 Malengo ya Somo la Mafunzo Kabilishi na Mjongeo 5

1.9 Upimaji na Tathmini 6

1.10 Muda wa Mafunzo 7

1.11 Maudhui ya Muhtasari wa Somo 7

2.0 Maudhui ya Muhtasari 8

2.1 Umahiri Mkuu na Umahiri Mahususi wa Somo 8

2.2 Maudhui ya Ufundishaji wa Somo 10

Majedwali

Jedwali namba 1: Upimaji Endelevu na Upimaji Tamati 6

Jedwali namba 2: Umahiri wa Somo la Mafunzo Kabilishi na Mjongeo kwa Mwalimu Tarajali wa Fani ya Ulemavu wa Uoni 8

Jedwali namba 3: Maudhui ya Ufundishaji wa Somo la Mafunzo Kabilishi na Mjongeo kwa Mwalimu Tarajali wa Fani ya Ulemavu wa Uoni 10

Orodha ya Machapisho 24

1.0 Taarifa za Awali

1.1 Utangulizi

Muhtasari huu wa somo la Mafunzo Kabilishi na Mjongeo umeandaliwa kutokana na Mtaala wa Mafunzo ya Ualimu Elimu Maalumu wa mwaka 2019. Muhtasari huu unalenga kumjengea mwalimu tarajali maarifa, stadi na mwelekeo utakaomwezesha kukabiliana na mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji wa mwanafunzi mwenye ulemavu wa uoni aliyedahiliwa katika elimu ya msingi.

Ili kumsaidia mkufunzi, yametolewa mapendekezo ya mbinu za kufundishia na kujifunzia, zana/vifaa vya kufundishia na kujifunzia pamoja na upimaji. Mkufunzi anahimizwa kutumia mbinu mbalimbali na zana zinazopatikana kwenye mazingira yanayohusika na upimaji ulioshauriwa kwenye muhtasari huu. Pamoja na mbinu zilizoainishwa kwenye muhtasari huu mkufunzi anaweza kutumia mbinu nyingine tofautitofauti kulingana na mazingira na mahitaji ya mwalimu tarajali na umahiri unaojengwa.

1.2 Muundo wa Muhtasari

Muhtasari huu umegawanyika katika sehemu kuu mbili. Sehemu ya kwanza ina taarifa za awali na sehemu ya pili ni maudhui ya muhtasari.

Sehemu ya kwanza inajumuisha utangulizi, muundo wa muhtasari, sababu za kuandaa muhtasari, malengo ya elimu nchini Tanzania, malengo ya jumla ya mafunzo ya astashahada ya ualimu elimu maalumu, madhumuni ya mafunzo ya astashahada ya ualimu elimu maalumu, umahiri wa jumla wa mafunzo ya astashahada ya ualimu elimu maalumu, malengo ya somo la Mafunzo Kabilishi na Mjongeo, upimaji na tathmini na muda wa mafunzo. Sehemu ya pili inajumuisha maudhui ya muhtasari wa somo.

1.3 Sababu za Kuandaa Muhtasari

Dira ya elimu na mafunzo inasisitiza kuwapo kwa mwalimu aliye bora kitaaluma na kitaalamu na mwenye mbinu mbalimbali za kufundishia na kujifunzia somo la Mafunzo Kabilishi na Mjongeo ili kukabiliana na changamoto za mahitaji na matarajio ya kielimu kulingana na mabadiliko ya sayansi na teknolojia.

Mwelekeo wa dira na mpango wa elimu kwa ujumla ni kumuandaa mwalimu mwenye ujuzi wa kumfundisha mwanafunzi mwenye ulemavu wa uoni katika shule za msingi kwa kuzingatia misingi, kanuni na mielekeo inayopasa. Mwalimu tarajali wa somo la Mafunzo Kabilishi na Mjongeo kwa ajili ya mwanafunzi mwenye ulemavu wa uoni anahitaji kupata ujuzi wa kuweza kuyatumia vema mazingira yake.

1.4 Malengo ya Elimu Nchini Tanzania

Elimu inayotolewa ni ya kurithisha maarifa, stadi na mielekeo bora kutoka kwa vizazi vilivyopita hadi vizazi vya wakati huu na vijavyo. Hivyo, yafuatayo ndiyo malengo makuu ya elimu nchini:

a) kuendeleza na kukuza maendeleo, kuboresha haiba ya wananchi wa Tanzania, rasilimali zao na matumizi bora ya rasilimali hizo katika kuleta maendeleo ya mtu binafsi na ya kitaifa;
b) kukuza tabia ya kuthamini utamaduni, mila na desturi za watanzania;
c) kukuza upatikanaji wa fursa za kusoma, kuandika na kuhesabu na matumizi sahihi ya maarifa na stadi za kijamii, kisayansi, kiufundi, kiteknolojia, kitaalamu na aina nyingine za maarifa na ujuzi, kwa ajili ya maendeleo na kuboresha hali ya mtu na jamii;
d) kukuza na kuendeleza kujiamini, kudadisi, weledi na kuheshimu utu wa mtu na haki za binadamu na kuwa tayari kufanya kazi kwa kujiendeleza na kwa maendeleo ya Taifa;
e) kuwezesha na kupanua mawanda ya kujipatia maarifa, kuboresha na kukuza stadi za kiakili, utendaji, uzalishaji na nyingine zinazotakiwa katika kukidhi mabadiliko ya mahitaji kiuchumi;

f) kumwezesha kila raia kuelewa misingi ya katiba ya nchi pamoja na kuthamini haki za binadamu na uraia, wajibu na majukumu yanayoendana nayo;
g) kukuza utashi wa kupenda na kuheshimu kazi za kujiajiri na kuajiriwa na kuboresha utendaji kazi katika sekta za uzalishaji na huduma;
h) kujenga misingi ya maadili yanayokubalika kitaifa na ushirikiano wa kitaifa na kimataifa, amani na sheria kwa njia ya kujifunza;
i) kuwezesha kuwapo kwa matumizi sahihi, usimamizi na utunzaji wa mazingira; na
j) kujenga tabia na utamaduni wa kuwakubali watu wenye ulemavu na kuwashirikisha kwenye nyanja zote za maisha kwa maendeleo ya Taifa.

1.5 Malengo ya Jumla ya Mafunzo ya Astashahada ya Ualimu Elimu Maalumu

Mafunzo ya Ualimu Elimu Maalumu yana malengo yafuatayo:

a) kumjengea umahiri mwalimu tarajali katika nadharia za saikolojia ya elimu, malezi, ushauri na huduma kwa watu wenye ulemavu;
b) kumjengea umahiri mwalimu tarajali katika kugundua na kubuni mbinu na njia za kufundishia na kujifunzia;
c) kumjengea umahiri mwalimu tarajali katika uchambuzi wa mtaala na vifaa vya mtaala;
d) kumjengea umahiri mwalimu tarajali katika kumudu stadi kuu za masomo ya lugha, sanaa na maendeleo ya sayansi na teknolojia;
e) kumjengea umahiri mwalimu tarajali katika kufanya upimaji na tathmini ya maendeleo katika elimu;
f) kumjengea umahiri mwalimu tarajali katika stadi za uongozi na utawala katika elimu; na
g) kumjengea umahiri mwalimu tarajali katika kumfundisha mwanafunzi mwenye mahitaji maalumu.

1.6 Madhumuni ya Mafunzo ya Astashahada ya Ualimu Elimu Maalumu

Mwishoni mwa mafunzo ya Astashahada ya Ualimu Elimu Maalumu ya muda wa miaka miwili, mwalimu tarajali aweze:

a) kutafsiri mtaala wa elimu ya msingi na mihtasari yake katika masomo darasani;
b) kuandaa na kutumia njia shirikishi katika ufundishaji na ujifunzaji kwa kuzingatia mahitaji ya mwanafunzi;
c) kubuni, kuendeleza na kufaragua zana za ufundishaji na ujifunzaji katika elimu ya msingi kwa kuzingatia mahitaji ya mwanafunzi;
d) kufanya tafiti tatuzi za kielimu ili kuwabaini, kuwaendeleza na kuwasaidia wanafunzi wenye mahitaji maalumu katika shule za msingi;
e) kurithisha desturi, maadili na tabia zinazokubalika kwa wanafunzi wa shule za msingi;
f) kuchagua, kupanga, kusimamia na kuongoza vipindi darasani katika shule za msingi;
g) kufundisha kwa ufanisi masuala mtambuka; na
h) kutunga na kusahihisha majaribio na mitihani inayoendana na mtaala wa elimu ya msingi kwa kuzingatia mahitaji ya mwanafunzi katika nyanja zote tatu za kujifunza.

1.7 Umahiri wa Jumla wa Mafunzo ya Astashahada ya Ualimu Elimu Maalumu

Umahiri mkuu wa mafunzo ya Astashahada ya Ualimu Elimu Maalumu umejikita katika kumuandaa mwalimu tarajali aweze:

a) kumbaini mwanafunzi mwenye mahitaji maalumu, kujenga misingi ya kukubalika kwa wenzake, kwa jamii na kumpatia afua stahiki;
b) kutumia mazingira wezeshi ya ufundishaji na ujifunzaji kwa mwanafunzi mwenye mahitaji maalumu;
c) kutumia njia mbalimbali za mawasiliano na teknolojia saidizi kwa kuzingatia mahitaji maalumu ya mwanafunzi;
d) kutumia mbinu mbalimbali katika kutambua vipaji walivyonavyo wanafunzi wenye mahitaji maalumu na namna ya kuviendeleza;

e) kufanya tafiti tatuzi za kielimu ili kuwabaini na kuwasaidia wanafunzi wenye mahitaji maalumu katika shule za msingi;
f) kutumia misingi na stadi za uongozi katika kuongoza taasisi mbalimbali za elimu;
g) kutumia, kutunza na kukarabati vifaa saidizi vya wanafunzi wenye mahitaji maalumu;
h) kutumia sanaa na michezo rekebifu katika kuibua na kuendeleza vipaji mbalimbali vya wanafunzi wenye mahitaji maalumu;
i) kutumia misingi ya ufundishaji na ujifunzaji kufundishia masomo ya taaluma;
j) kujenga umahiri wa masomo kwa mwalimu tarajali utakaomwezesha kuelewa masomo vema na hivyo kumfundisha mwanafunzi mwenye mahitaji maalumu; na
k) kushirikiana na familia za wanafunzi wenye mahitaji maalumu katika kuwajengea wanafunzi hao kujiamini, tabia ya kujifunza na kukuza vipaji walivyonavyo.

1.8 Malengo ya Somo la Mafunzo Kabilishi na Mjongeo

Somo la Mafunzo Kabilishi na Mjongeo linamuandaa mwalimu tarajali wa elimu maalumu ili aweze:

a) kumjengea mwanafunzi uwezo wa kutumia stadi za mafunzo kabilishi na ujongeaji ili ayamudu mazingira yake;
b) kumjengea mwanafunzi uwezo wa kutumia mbinu za ujongeaji binafsi na zile za matumizi ya vifaa saidizi ili kupunguza utegemezi;
c) kutumia stadi za mafunzo kabilishi na mjongeo kumjengea mwanafunzi stadi za maisha; na
d) kuwawezesha walimu, wazazi na wanafunzi kutumia stadi za ukabilishi na mjongeo kuwezesha wanafunzi wenye ulemavu wa uoni kumudu mazingira.

1.9 Upimaji na Tathmini

Muhtasari huu umependekeza mbinu mbalimbali za upimaji na tathmini kwa kuzingatia mahitaji ya mwalimu tarajali wakati wa mchakato wa ujifunzaji wa kozi ya ualimu. Upimaji tamati utafanywa na Baraza la Mitihani la Tanzania na utakuwa na alama 50. Upimaji endelevu utafanywa na mkufunzi wakati mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji unaendelea na utakuwa na alama 50. Upimaji huu unahusisha majaribio, kazimradi, kazi binafsi, mkoba wa kazi, kazi kwa vitendo na mtihani wa mwisho wa muhula. Uzito wa kila aina ya upimaji umeoneshwa katika jedwali lifuatalo:

Jedwali namba 1: Upimaji Endelevu na Upimaji Tamati

Vipengele	**Njia za Upimaji**	**Mwaka**				**Idadi**	**Alama (%)**
		Mwaka wa I		**Mwaka wa II**			
		Muhula wa I	**Muhula wa II**	**Muhula wa I**	**Muhula wa II**		
Taaluma	Majaribio	1	1	1	1	4	10
	Kazimradi	1	-	1	-	2	5
	Kazi binafsi	1	1	1	-	3	5
	Kazi kwa vitendo	1	1	1	-	3	5
	Mkoba wa kazi	1	-	1	-	2	5
	Mtihani wa mwisho wa muhula	1	1	1		3	20
Upimaji endelevu							50
Upimaji tamati: Mtihani wa Baraza la Mitihani la Tanzania					1	1	50
Jumla ya alama za upimaji endelevu na upimaji tamati							**100**

1.10 Muda wa Mafunzo

Muhtasari huu wa somo la Mafunzo Kabilishi na Mjongeo kwa fani ya ulemavu wa uoni umekusudiwa kukamilishwa kwa kipindi cha miaka miwili. Mtazamo wa somo hili ni kumjengea mwalimu tarajali misingi muhimu ya maarifa ya somo la Mafunzo Kabilishi na Mjongeo itakayomwezesha kufundisha kikamilifu mwanafunzi mwenye ulemavu wa uoni kumudu ujifunzaji katika elimu ya msingi.

1.11 Maudhui ya Muhtasari wa Somo

Maudhui ya muhtasari yamepangwa katika jedwali yakihusisha umahiri mkuu, umahiri mahususi, shughuli za kutendwa na mwalimu tarajali, vigezo vya upimaji, viwango vya utendaji na idadi ya vipindi

1.11.1 Umahiri

Ni uwezo wa kufikiri na kutenda kwa ufanisi

1.11.2 Umahiri Mkuu

Ni uwezo wa kutenda jambo kwa usahihi na ufanisi unaokusudiwa kufikiwa na mwalimu tarajali baada ya kujifunza kwa muda fulani. Hujengwa na umahiri mahususi atakaojengewa mwalimu tarajali kwa kutenda shughuli mbalimbali

1.11.3 Umahiri Mahususi

Ni uwezo atakaojengewa mwalimu tarajali katika kutenda shughuli mbalimbali kwa muda maalumu

1.11.4 Shughuli za Kutendwa na Mwalimu Tarajali

Ni vitendo ambavyo mwalimu tarajali anapaswa kuvifanya ili kufikia umahiri mahususi uliokusudiwa

1.11.5 Vigezo vya Upimaji

Ni viwango vya ufanisi wa utendaji wa mwalimu tarajali ili kufikia umahiri mahususi

1.11.6 Viwango vya Utendaji

Ni kiasi cha ufikiwaji wa vigezo vya kila shughuli anayotenda mwalimu tarajali

1.11.7 Idadi ya Vipindi

Idadi ya vipindi ni makadirio ya muda utakaotumika katika kufundisha na kujifunza kwa kuzingatia uzito wa umahiri mahususi na shughuli za kutendwa na mwalimu tarajali. Makadirio haya ya muda yamewekwa kwa mfumo wa vipindi ambapo kila kipindi ni dakika 60. Somo hili litafundishwa kwa vipindi viwili (2) kwa wiki. Hata hivyo, mapendekezo haya ya idadi ya vipindi yanaweza kubadilika kulingana na mazingira ya kufundishia na kujifunzia.

2.0 Maudhui ya Muhtasari

2.1 Umahiri Mkuu na Umahiri Mahususi wa Somo

Jedwali namba 2: Umahiri wa Somo la Mafunzo Kabilishi na Mjongeo kwa Mwalimu Tarajali wa Fani ya Ulemavu wa Uoni

Umahiri Mkuu	Umahiri Mahususi
1.0 Kutumia stadi za mafunzo kabilishi kumwezesha mwanafunzi mwenye ulemavu wa uoni kuyamudu mazingira	1.1 Kujenga uwezo wa kutumia stadi za mafunzo kabilishi kumwezesha mwanafunzi mwenye ulemavu wa uoni kuyamudu mazingira yake 1.2 Kutumia stadi za mafunzo kabilishi kukuza hisi za milangobaki ya fahamu kwa mwanafunzi mwenye ulemavu wa uoni

Umahiri Mkuu	Umahiri Mahususi
	1.3 Kujenga stadi za kujitambua binafsi na kujikubali kwa mwanafunzi
2.0 Kujenga stadi za ujongeaji ili kumwezesha mwanafunzi mwenye ulemavu wa uoni kuyamudu mazingira	2.1 Kuchambua maeneo/sehemu za mafunzo ya mjongeo kwa mwanafunzi mwenye ulemavu wa uoni 2.2 Kujenga stadi za ujongeaji huru 2.3 Kuchambua mifumo ya ujongeaji katika kujenga stadi za mjongeo
3.0 Kutumia stadi za mafunzo kabilishi na mjongeo kujenga stadi za maisha kwa mwanafunzi mwenye ulemavu wa uoni	3.1 Kuchambua stadi za maisha kwa mwanafunzi mwenye ulemavu wa uoni 3.2 Kujenga stadi za kijamii kwa mwanafunzi mwenye ulemavu wa uoni 3.3 Kujenga stadi za kiuchumi kwa mwanafunzi mwenye ulemavu wa uoni

2.2 Maudhui ya Ufundishaji wa Somo

Jedwali namba 3: Maudhui ya Ufundishaji wa Somo la Mafunzo Kabilishi na Mjongeo kwa Mwalimu Tarajali wa Fani ya Ulemavu wa Uoni

Umahiri Mkuu	Umahiri Mahususi	Shughuli za Kutendwa na Mwalimu Tarajali	Vigezo vya Upimaji	Viwango vya Utendaji kwa Mwalimu Tarajali				Idadi ya Vipindi
				Utendaji Chini ya Wastani	Utendaji wa Wastani	Utendaji Mzuri	Utendaji Mzuri Sana	
1.0 Kutumia stadi za mafunzo kabilishi kumwezesha mwanafunzi mwenye ulemavu wa uoni kuyamudu mazingira	1.1 Kujenga uwezo wa kutumia stadi za mafunzo kabilishi kumwezesha mwanafunzi mwenye ulemavu wa uoni kuyamudu mazingira yake	a) Kufafanua dhana ya mafunzo kabilishi	Dhana ya mafunzo kabilishi (maana na umuhimu) imefafanuliwa.	Anafafanua dhana ya mafunzo kabilishi kwa kuzingatia maana.	Anafafanua dhana ya mafunzo kabilishi kwa kuzingatia maana na umuhimu.	Anafafanua dhana ya mafunzo kabilishi kwa kuzingatia maana, umuhimu na kutoa mifano.	Anafafanua dhana ya mafunzo kabilishi kwa kuzingatia maana, umuhimu, kutoa mifano na kuhusisha na maisha ya kila siku.	10
		b) Kubaini kanuni za mafunzo kabilishi	Kanuni za mafunzo kabilishi zimebainishwa.	Anabainisha kanuni moja ya mafunzo kabilishi.	Anabainisha kanuni mbili za mafunzo kabilishi.	Anabainisha kanuni tatu za mafunzo kabilishi.	Anabainisha kanuni tatu za mafunzo kabilishi na kueleza umuhimu wake.	

Umahiri Mkuu	Umahiri Mahususi	Shughuli za Kutendwa na Mwalimu Tarajali	Vigezo vya Upimaji	Viwango vya Utendaji kwa Mwalimu Tarajali				Idadi ya Vipindi
				Utendaji Chini ya Wastani	Utendaji wa Wastani	Utendaji Mzuri	Utendaji Mzuri Sana	
		c) Kuchambua maeneo/sehemu za mafunzo kabilishi	Maeneo/sehemu za mafunzo kabilishi zimechambuliwa.	Anachambua eneo/sehemu moja ya mafunzo kabilishi.	Anachambua maeneo/ sehemu mbili za mafunzo kabilishi.	Anachambua maeneo/sehemu tatu za mafunzo kabilishi na kutoa mifano.	Anachambua maeneo/sehemu tatu za mafunzo kabilishi, kutoa mifano na kuonesha uhalisia wa kimatumizi.	
	1.2 Kutumia stadi za mafunzo kabilishi kukuza hisi za milangobaki ya fahamu kwa mwanafunzi mwenye ulemavu wa uoni	a) Kubaini mbinu za ukuzaji wa hisi za milangobaki ya fahamu kwa mwanafunzi mwenye ulemavu wa uoni	Mbinu za ukuzaji wa hisi za milangobaki ya fahamu zimebainishwa.	Anabainisha mbinu mbili za ukuzaji wa hisi za milangobaki ya fahamu.	Anabainisha mbinu tatu za ukuzaji wa hisi za milangobaki ya fahamu.	Anabainisha mbinu nne za ukuzaji wa hisi za milangobaki ya fahamu.	Anabainisha mbinu tano za ukuzaji wa hisi za milangobaki ya fahamu na kuelezea umuhimu wake.	10
		b) Kufafanua stadi za mafunzo kabilishi kukuza hisi za milangobaki ya fahamu	Maelezo ya kuainisha stadi za mafunzo kabilishi ili kukuza hisi za milangobaki ya fahamu yametolewa.	Anatoa maelezo ya kuainisha stadi moja ya kukuza hisi za milangobaki ya fahamu.	Anatoa maelezo ya kuainisha stadi mbili za kukuza hisi za milangobaki ya fahamu.	Anatoa maelezo ya kuainisha stadi tatu za kukuza hisi za milangobaki ya fahamu.	Anatoa maelezo ya kuainisha stadi nne za kukuza hisi za milangobaki ya fahamu na kuelezea umuhimu wake.	

Umahiri Mkuu	Umahiri Mahususi	Shughuli za Kutendwa na Mwalimu Tarajali	Vigezo vya Upimaji	Viwango vya Utendaji kwa Mwalimu Tarajali				Idadi ya Vipindi
				Utendaji Chini ya Wastani	Utendaji wa Wastani	Utendaji Mzuri	Utendaji Mzuri Sana	
		c) Kutumia hisi za milangobaki ya fahamu kubaini maeneo, vitu, na hali	Hisi za milango baki ya fahamu zimetumika.	Anatumia hisi za milango baki ya fahamu kubaini maeneo.	Anatumia hisi za milangobaki ya fahamu kubaini maeneo na vitu.	Anatumia hisi za milangobaki ya fahamu kubaini maeneo, vitu na hali.	Anatumia hisi za milangobaki ya fahamu kubaini maeneo, vitu, hali na kuonesha umuhimu wake.	
	1.3 Kujenga stadi za kujitambua binafsi na kujikubali kwa mwanafunzi	a) Kufafanua sehemu za nje za mwili wa binadamu kwa kutumia hatua na mbinu mbalimbali	Sehemu za nje za mwili wa binadamu zimefafanuliwa.	Anatumia hatua na mbinu mbalimbali kutaja kazi za sehemu mbili za nje za mwili wa binadamu.	Anatumia hatua na mbinu mbalimbali kutaja na kufafanua kazi za sehemu tatu za nje za mwili wa binadamu	Anatumia hatua na mbinu mbalimbali kutaja na kufafanua kazi za sehemu tano za nje za mwili wa binadamu.	Anatumia hatua na mbinu mbalimbali kutaja na kufafanua kazi za sehemu saba za nje za mwili wa binadamu	12
		b) Kujenga stadi za uvaaji	Stadi za uvaaji zimejengwa.	Anabaini vifaa vya mafunzo ya uvaaji.	Anabaini vifaa na aina za mavazi katika mafunzo ya uvaaji.	Anabaini vifaa, aina za mavazi na hatua za mafunzo ya uvaaji na kukazia maarifa ya mafunzo.	Anabaini vifaa, aina za mavazi, hatua na mbinu mbadala za mafunzo ya uvaaji na kukazia maarifa ya mafunzo.	

Umahiri Mkuu	Umahiri Mahususi	Shughuli za Kutendwa na Mwalimu Tarajali	Vigezo vya Upimaji	Viwango vya Utendaji kwa Mwalimu Tarajali				Idadi ya Vipindi
				Utendaji Chini ya Wastani	Utendaji wa Wastani	Utendaji Mzuri	Utendaji Mzuri Sana	
		c) Kumwezesha mwanafunzi kuoga kwa kubaini tahadhari za vifaa na hatua	Vifaa, hatua, mambo ya kuzingatia na tahadhari zimebainishwa.	Anabaini vifaa vya kutumia wakati wa kuoga.	Anabaini vifaa na hatua za kufuata wakati wa kuoga.	Anabaini vifaa, hatua na mambo ya kuzingatia wakati wa kuoga.	Anabaini vifaa, hatua mambo ya kuzingatia na tahadhari za kuchukua wakati wa kuoga.	
		d) Kubaini vifaa na hatua za kupaka mafuta mwilini kwa mwanafunzi	Vifaa na hatua za kupaka mafuta mwilini zimebainishwa.	Anabaini vifaa vya kumwezesha mwanafunzi kupaka mafuta mwilini.	Anabaini vifaa na kufafanua hatua za kupaka mafuta mwilini.	Anabaini vifaa, kufafanua hatua, mambo ya kuzingatia na tahadhari za kuchukua katika kupaka mafuta mwilini.	Anabaini vifaa, kufafanua hatua, mambo ya kuzingatia na tahadhari za kuchukua wakati wa kupaka mafuta mwilini kwa kutoa mifano.	

Umahiri Mkuu	Umahiri Mahususi	Shughuli za Kutendwa na Mwalimu Tarajali	Vigezo vya Upimaji	Viwango vya Utendaji kwa Mwalimu Tarajali				Idadi ya Vipindi
				Utendaji Chini ya Wastani	Utendaji wa Wastani	Utendaji Mzuri	Utendaji Mzuri Sana	
2.0 Kujenga stadi za ujongeaji ili kumwezesha mwanafunzi mwenye ulemavu wa uoni kuyamudu mazingira	2.1 Kuchambua maeneo/sehemu za mafunzo ya mjongeo kwa mwanafunzi mwenye ulemavu wa uoni	a) Kuelezwa kwa dhana ya ujongeaji	Dhana ya mafunzo ya ujongeaji imeelezwa.	Anaeleza dhana ya mafunzo ya ujongeaji kwa kuzingatia maana.	Anaeleza dhana ya mafunzo ya ujongeaji kwa kuzingatia maana na historia.	Anaeleza dhana ya mafunzo ya ujongeaji kwa kuzingatia maana, historia na umuhimu.	Anaeleza dhana ya mafunzo ya ujongeaji kwa kuzingatia maana, historia, umuhimu na kubaini changamoto za mafunzo hayo katika nchi zinazoendelea.	13
		b) Kufafanuliwa kwa dhana ya alama za kudumu	Dhana ya alama za kudumu imefafanuliwa.	Anafafanua dhana ya alama za kudumu kwa kuzingatia maana na vitu viwili.	Anafafanua dhana ya alama za kudumu kwa kuzingatia maana na vitu vinne.	Anafafanua dhana ya alama za kudumu kwa kuzingatia maana, vitu vitano na kubaini umuhimu wake.	Anafafanua dhana ya alama za kudumu kwa kuzingatia maana, vitu sita na kubaini umuhimu na kanuni za utumiaji wa alama hizo.	

Umahiri Mkuu	Umahiri Mahususi	Shughuli za Kutendwa na Mwalimu Tarajali	Vigezo vya Upimaji	Viwango vya Utendaji kwa Mwalimu Tarajali				Idadi ya Vipindi
				Utendaji Chini ya Wastani	Utendaji wa Wastani	Utendaji Mzuri	Utendaji Mzuri Sana	
		c) Kufafanua dhana ya alama zisizo za kudumu (vidokezo)	Dhana ya alama zisizo za kudumu (vidokezo) imefafanuliwa.	Anafafanua dhana ya alama zisizo za kudumu (vidokezo) kwa kuzingatia maana na aina mbili.	Anafafanua dhana ya alama zisizo za kudumu (vidokezo) kwa kuzingatia maana na aina tatu.	Anafafanua dhana ya alama zisizo za kudumu (vidokezo) kwa kuzingatia maana, aina nne na umuhimu.	Anafafanua dhana ya alama zisizo za kudumu (vidokezo) kwa kuzingatia maana, aina tano, umuhimu na kanuni za matumizi ya alama hizo.	
		d) Kuchambua vipimo katika kujenga stadi za mjongeo kwa kuzingatia ramani	Vipimo katika kujenga stadi za mjongeo kwa kuzingatia ramani vimechambuliwa.	Anachambua vipimo kwa kuzingatia vipimo rasmi.	Anachambua vipimo kwa kuzingatia vipimo rasmi na visivyo rasmi.	Anachambua vipimo kwa kuzingatia vipimo rasmi na visivyo rasmi na vya ulinganishi na kutoa mifano.	Anachambua vipimo kwa kuzingatia vipimo rasmi, visivyo rasmi, vya ulinganishi, kutoa mifano na kubaini umuhimu wake.	

Umahiri Mkuu	Umahiri Mahususi	Shughuli za Kutendwa na Mwalimu Tarajali	Vigezo vya Upimaji	Viwango vya Utendaji kwa Mwalimu Tarajali				Idadi ya Vipindi
				Utendaji Chini ya Wastani	Utendaji wa Wastani	Utendaji Mzuri	Utendaji Mzuri Sana	
		e) Kubainisha matumizi ya dira katika kujenga stadi za mjongeo	Matumizi ya dira katika kujenga stadi za mjongeo yamebainishwa.	Anabainisha matumizi ya dira kwa kuzingatia pande kuu mbili za dunia.	Anabainisha matumizi ya dira kwa kuzingatia pande kuu tatu za dunia.	Anabainisha matumizi ya dira kwa kuzingatia pande kuu nne za dunia.	Anabainisha matumizi ya dira kwa kuzingatia pande kuu nne za dunia na kutoa mifano.	
		f) Kufafanua dhana ya kuyatambua mazingira	Dhana ya kuyatambua mazingira imefafanuliwa.	Anafafanua dhana ya kuyatambua mazingira kwa kuzingatia maana na aina moja ya mazingira.	Anafafanua dhana ya kuyatambua mazingira kwa kuzingatia maana na aina mbili za mazingira.	Anafafanua dhana ya kuyatambua mazingira kwa kuzingatia maana na aina tatu za mazingira.	Anafafanua dhana ya kuyatambua mazingira kwa kuzingatia maana, aina tatu za mazingira na kubaini umuhimu wa kuyatambua mazingira.	
	2.2 Kujenga stadi za ujongeaji huru	a) Kueleza dhana ya ujongeaji huru (maana, mambo ya kuzingatia na umuhimu)	Dhana ya ujongeaji huru imeelezwa.	Anaeleza dhana ya ujongeaji huru kwa kuzingatia maana.	Anaeleza dhana ya ujongeaji huru kwa kuzingatia maana na mambo ya kuzingatia.	Anaeleza dhana ya ujongeaji huru kwa kuzingatia maana, mambo ya kuzingatia na umuhimu.	Anaeleza dhana ya ujongeaji huru kwa kuzingatia maana, mambo ya kuzingatia, umuhimu na kutoa mifano.	10

Umahiri Mkuu	Umahiri Mahususi	Shughuli za Kutendwa na Mwalimu Tarajali	Vigezo vya Upimaji	Viwango vya Utendaji kwa Mwalimu Tarajali				Idadi ya Vipindi
				Utendaji Chini ya Wastani	Utendaji wa Wastani	Utendaji Mzuri	Utendaji Mzuri Sana	
		b) Kufafanua mbinu ya kulinda sehemu za mwili (maana, aina, mambo ya kuzingatia, faida na hasara)	Mbinu za kujilinda zimefafanuliwa.	Anafafanua mbinu za kujilinda kwa kuzingatia maana na aina moja.	Anafafanua mbinu za kujilinda kwa kuzingatia maana na aina mbili.	Anafafanua mbinu za kujilinda kwa kuzingatia maana, aina mbili na mambo ya kuzingatia.	Anafafanua mbinu za kujilinda kwa kuzingatia maana aina mbili, mambo ya kuzingatia, faida na hasara za mbinu hizo.	
		c) Kuchanganua mbinu za kutembea kwa kugusa	Mbinu za kutembea kwa kugusa zimechanganuliwa.	Anachanganua mbinu moja ya kutembea kwa kugusa na kutoa mfano.	Anachanganua mbinu mbili za kutembea kwa kugusa na kutoa mifano.	Anachanganua mbinu tatu za kutembea kwa kugusa na kutoa mifano.	Anachanganua mbinu nne za kutembea kwa kugusa na kutoa mifano.	
	2.3 Kuchambua mfumo wa ujongeaji katika kujenga stadi za mjongeo	a) Kueleza dhana ya mtu mwongozaji	Dhana ya mtu mwongozaji kwa kuzingatia maana, mambo ya kuzingatia, mbinu kulingana na eneo la uongozaji, faida na hasara imeelezwa.	Anaeleza dhana ya mtu mwongozaji kwa kuzingatia maana, mambo ya kuzingatia na mbinu kulingana na maeneo mawili ya uongozaji.	Anaeleza dhana ya mtu mwongozaji kwa kuzingatia maana, mambo ya kuzingatia na mbinu kulingana na maeneo manne ya uongozaji.	Anaeleza dhana ya mtu mwongozaji kwa kuzingatia maana, mambo ya kuzingatia na mbinu kulingana na maeneo sita ya uongozaji.	Anaeleza dhana ya mtu mwongozaji kwa kuzingatia maana, mambo ya kuzingatia na mbinu kulingana na maeneo sita ya uongozaji na kubainisha faida na hasara za mbinu hii.	12

Umahiri Mkuu	Umahiri Mahususi	Shughuli za Kutendwa na Mwalimu Tarajali	Vigezo vya Upimaji	Viwango vya Utendaji kwa Mwalimu Tarajali				Idadi ya Vipindi
				Utendaji Chini ya Wastani	Utendaji wa Wastani	Utendaji Mzuri	Utendaji Mzuri Sana	
		b) Kufafanua mbinu ya kutembea kwa kutumia fimbo nyeupe	Mbinu ya kutembea kwa kutumia fimbo nyeupe imefafanuliwa kwa kuzingatia maana, aina, sifa, mambo ya kuzingatia katika kutumia, faida na hasara.	Anafafanua mbinu ya kutembea kwa kutumia fimbo nyeupe kwa kuzingatia maana na aina za fimbo nyeupe.	Anafafanua mbinu ya kutembea kwa kutumia fimbo nyeupe kwa kuzingatia maana, aina na sifa.	Anafafanua mbinu ya kutembea kwa kutumia fimbo nyeupe kwa kuzingatia maana, aina, sifa, mambo ya kuzingatia katika kutumia fimbo nyeupe, faida na hasara.	Anafafanua mbinu ya kutembea kwa kutumia fimbo nyeupe kwa kuzingatia maana, aina, sifa, mambo ya kuzingatia katika kutumia fimbo nyeupe, faida, hasara na kutoa mifano.	
		c) Kufafanua mbinu ya mbwa mwongozaji	Mbinu ya mbwa mwongozaji imefafanuliwa kwa kuzingatia maana, mambo ya kuzingatia, vikwazo vya matumizi katika nchi zinazoendelea, faida na hasara zake.	Anafafanua mbinu ya mbwa mwongozaji kwa kuzingatia maana na mambo ya kuzingatia.	Anafafanua mbinu ya mbwa mwongozaji kwa kuzingatia maana, mambo ya kuzingatia na vikwazo vya matumizi katika nchi zinazoendelea.	Anafafanua mbinu ya mbwa mwongozaji kwa kuzingatia maana, mambo ya kuzingatia, vikwazo vya matumizi katika nchi zinazoendelea na faida zake.	Anafafanua mbinu ya mbwa mwongozaji kwa kuzingatia maana, mambo ya kuzingatia, vikwazo vya matumizi katika nchi zinazoendelea, faida na hasara zake.	

Umahiri Mkuu	Umahiri Mahususi	Shughuli za Kutendwa na Mwalimu Tarajali	Vigezo vya Upimaji	Viwango vya Utendaji kwa Mwalimu Tarajali				Idadi ya Vipindi
				Utendaji Chini ya Wastani	Utendaji wa Wastani	Utendaji Mzuri	Utendaji Mzuri Sana	
3.0 Kutumia stadi za mafunzo kabilishi na mjongeo kujenga stadi za maisha kwa mwanafunzi mwenye ulemavu wa uoni	3.1 Kuchambua stadi za maisha kwa mwanafunzi mwenye ulemavu wa uoni	a) Kufafanua dhana ya stadi za maisha kwa mwanafunzi mwenye ulemavu wa uoni	Maana, aina na umuhimu wa stadi za maisha kwa mwanafunzi mwenye ulemavu wa uoni zimefafanuliwa.	Anafafanua maana na aina mbili za stadi za maisha.	Anafafanua maana na aina tatu za stadi za maisha.	Anafafanua maana na aina nne za stadi za maisha na umuhimu wake.	Anafafanua maana, aina nne za stadi za maisha, umuhimu wake na kubaini athari za kukosa stadi hizo.	13
		b) Kufafanua kanuni za mafunzo ya stadi za maisha kwa mwanafunzi mwenye ulemavu wa uoni	Kanuni za mafunzo ya stadi za maisha zimefafanuliwa.	Anafafanua kanuni moja ya mafunzo ya stadi za maisha.	Anafafanua kanuni mbili za mafunzo ya stadi za maisha.	Anafafanua kanuni tatu za mafunzo ya stadi za maisha.	Anafafanua kanuni nne za mafunzo ya stadi za maisha na kutoa mifano vijenzi vya kanuni hizo.	

Umahiri Mkuu	Umahiri Mahususi	Shughuli za Kutendwa na Mwalimu Tarajali	Vigezo vya Upimaji	Viwango vya Utendaji kwa Mwalimu Tarajali				Idadi ya Vipindi
				Utendaji Chini ya Wastani	Utendaji wa Wastani	Utendaji Mzuri	Utendaji Mzuri Sana	
		c) Kufafanua stadi za kiafya kwa mwanafunzi mwenye ulemavu wa uoni	Usafi wa mwili na mazingira umefafanuliwa.	Anafafanua dhana ya usafi wa mwili.	Anafafanua dhana ya usafi wa mwili, anataja hatua kwa hatua vitendo vya usafi wa mwili.	Anafafanua dhana ya usafi wa mwili, anataja hatua kwa hatua vitendo vya usafi wa mwili na usafi wa mazingira.	Anafafanua dhana ya usafi wa mwili, anataja hatua kwa hatua vitendo vya usafi wa mwili na usafi wa mazingira na kubaini umuhimu wake.	
		d) Kuainisha shughuli za kiuchumi kwa mwanafunzi mwenye ulemavu wa uoni	Stadi za kilimo, ufugaji, ufundi na biashara ndogondogo zimeainishwa.	Anaainisha stadi za kilimo.	Anaainisha stadi za kilimo na ufugaji.	Anaainisha stadi za kilimo, ufugaji na ufundi.	Anaainisha stadi za kilimo, ufugaji, ufundi na biashara.	

Umahiri Mkuu	Umahiri Mahususi	Shughuli za Kutendwa na Mwalimu Tarajali	Vigezo vya Upimaji	Viwango vya Utendaji kwa Mwalimu Tarajali				Idadi ya Vipindi
				Utendaji Chini ya Wastani	Utendaji wa Wastani	Utendaji Mzuri	Utendaji Mzuri Sana	
		e) Kueleza shughuli za kijamii anazoweza kushiriki mwanafunzi mwenye ulemavu wa uoni	Shughuli za kijamii anazoweza kushiriki mwanafunzi mwenye ulemavu wa uoni zimeelezwa.	Anaeleza shughuli mbili za kijamii.	Anaeleza shughuli tatu za kijamii.	Anaeleza shughuli nne za kijamii kwa kutoa mifano.	Anaeleza shughuli tano za kijamii na kubainisha umuhimu wake kwa kutoa mifano kulingana na mazingira.	
	3.2 Kujenga stadi za kijamii kwa mwanafunzi mwenye ulemavu wa uoni	a) Kubaini stadi za kijamii	Stadi za kijamii zimebainishwa.	Anabainisha stadi za kijamii kwa kuzingatia maana.	Anabainisha maana na aina ya stadi za kijamii.	Anabainisha maana, aina na umuhimu wa stadi za kijamii.	Anabainisha maana, aina na umuhimu wa stadi za kijamii na kutoa mifano.	14
		b) Kuelezea stadi tano za kula kwa mwanafunzi mwenye ulemavu wa uoni	Stadi tano za kula kwa mwanafunzi mwenye ulemavu wa uoni zimeelezewa.	Anaelezea stadi mbili za kula.	Anaelezea stadi tatu za kula.	Anaelezea stadi nne za kula.	Anaelezea stadi tano za kula na kubainisha umuhimu wake.	
		c) Kubainisha hatua za uvaaji	Hatua za kuvaa zimebainishwa.	Anabainisha hatua mbili za uvaaji.	Anabainisha hatua tatu za uvaaji.	Anabainisha hatua nne za uvaaji.	Anabainisha hatua tano za uvaaji na kutoa mifano.	

Umahiri Mkuu	Umahiri Mahususi	Shughuli za Kutendwa na Mwalimu Tarajali	Vigezo vya Upimaji	Viwango vya Utendaji kwa Mwalimu Tarajali				Idadi ya Vipindi
				Utendaji Chini ya Wastani	Utendaji wa Wastani	Utendaji Mzuri	Utendaji Mzuri Sana	
		d) Kuelezea hatua za kufua nguo kwa mwanafunzi mwenye ulemavu wa uoni	Hatua za kufua nguo kwa mwanafunzi mwenye ulemavu wa uoni zimeelezewa.	Anaelezea vifaa na hatua za kufua.	Anaelezea vifaa na hatua za kufua, kuanika na kuanua nguo.	Anaelezea vifaa na hatua za kufua, kuanika, kuanua na kukunja nguo.	Anaelezea vifaa na hatua za kufua, kuanika, kuanua na kukunja nguo kwa kutoa mifano kulingana na mazingira halisi.	
		e) Kubainisha hatua za kupiga pasi kwa mwanafunzi mwenye ulemavu wa uoni	Hatua za kupiga pasi kwa mwanafunzi mwenye ulemavu wa uoni zimebainishwa.	Anabainisha aina ya pasi na unamu wa nguo.	Anabainisha aina ya pasi, unamu wa nguo na sehemu za nguo.	Anabainisha aina ya pasi, unamu wa nguo, sehemu za nguo, sehemu ya kuanzia na ile ya kumalizia.	Anabainisha aina ya pasi, unamu wa nguo, sehemu za nguo, sehemu ya kuanzia, kumalizia na kubaini mambo ya kuzingatia kulingana na hali ya nguo.	

Umahiri Mkuu	Umahiri Mahususi	Shughuli za Kutendwa na Mwalimu Tarajali	Vigezo vya Upimaji	Viwango vya Utendaji kwa Mwalimu Tarajali				Idadi ya Vipindi
				Utendaji Chini ya Wastani	Utendaji wa Wastani	Utendaji Mzuri	Utendaji Mzuri Sana	
	3.3 Kujenga stadi za kiuchumi kwa mwanafunzi mwenye ulemavu wa uoni	a) Kuonesha mbinu za kubaini fedha	Mbinu za kubaini fedha zimeoneshwa.	Anatumia unamu na mlio kubaini fedha.	Anatumia unamu, umbo na mlio kubaini fedha.	Anatumia unamu, umbo, ukubwa na mlio kubaini fedha.	Anatumia unamu, umbo, ukubwa na mlio kubaini fedha za noti na sarafu na kubainisha tofauti.	10
		b) Kufafanua mbinu za kufanya ununuzi kwa mwanafunzi mwenye ulemavu wa uoni	Mbinu za ununuzi zimefafanuliwa.	Anafafanua mbinu nne za ununuzi.	Anafafanua mbinu tano za ununuzi.	Anafafanua mbinu sita za ununuzi.	Anafafanua mbinu saba za ununuzi kwa mifano.	
		c) Kueleza mambo ya kuzingatia katika kupanga bajeti	Mambo ya kuzingatia katika kupanga bajeti yameelezwa kwa ufasaha.	Anaeleza ubora wa bidhaa na kiasi cha fedha.	Anaeleza ubora wa bidhaa, kiasi cha fedha na kiasi cha mahitaji.	Anaeleza ubora wa bidhaa, kiasi cha fedha, kiasi cha mahitaji na muda wa matumizi.	Anaeleza ubora wa bidhaa, kiasi cha fedha, kiasi cha mahitaji, muda wa matumizi na kubainisha umuhimu wa kupanga bajeti.	

Orodha ya Machapisho

Beggs, W. D. A. (1992). Coping, adjustment, and mobility related feelings of newly visually impaired young adults. *Journal of Visual Impairment & Blindness, 86* (3), 136–140.

Fazzi, D., & Barlow, J. (2017). *Orientation and mobility techniques: A guide for the practitioner* (2nd ed.). New York, United States of America: AFB Press.

Hatlen, P. (1996). The core curriculum for blind and visually impaired students, including those with additional disabilities. *Review, 28* (1), 25-32.

Jacobson, W. H. (1993). *The art and science of teaching orientation and mobility to persons with visual impairment.* New York, United States of America: AFB Press.

Kenya Institute of Curriculum Development. (2013). *Community based education foundation level syllabuses for learners who are deafblind*. Nairobi, Kenya: KICD.